**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI**

# MARUDIO

# TANGAZO LA ZABUNI

## MWALIKO WA MAOMBI YA ZABUNI YA UPANGAJI WA VIBANDA KATIKA STENDI YA MABASI MASANGA KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**TAREHE:21/08/2019**

Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji inapenda inawatangazia na inawakaribisha Wamiliki wa kampuni za usafirishaji na mawakala wa usafirishaji kupanga vibanda katika stendi ya mabasi Masanga.

| NAMBA YA ZABUNI | AINA YA ZABUNI | GHARAMA YA MAOMBI KWA KILA ZABUNI | WANAOSTAHILI |
|---|---|---|---|
| LGA/042/2019/2020/NC/16 | Upangaji wa vibanda vya kukatia tiketi standi ya mabasi Masanga vibanda namba 1,3,4,7,8,11,12,13,15,16,17,22,23,24,25,26,30,31, 34,35 | **TZS 30,000.00** | Kampuni za Usafirishaji, Mawakala wa usafirishaji |

Mwombaji anatakiwa kuambatanisha nyaraka zifuatazo;-

1. Kivuli cha Leseni ya Biashara halali na iliyo hai ya usafirishaji kwa makampuni na leseni hai ya biashara ya uwakala wa usafirishaji kwa Mawakala
2. Kivuli cha Cheti cha usajili (Certificate of Registration) kwa Kampuni.
3. Kivuli cha Utambulisho wa mlipa kodi (TIN namba au VAT).
4. Aweke stakabadhi halisi ya malipo ya maombi.
5. Hati halisi ya uthibitisho wa uwakilishi wa ki-sheria (Power of attorney) kwa Makampuni tu -
6. Kivuli cha Hati ya kiapo (Affidavit form) kutoka Mahakamani kuwa mpangaji si mtumishi wala diwani wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

7. Kivuli cha Taarifa za kibenki (Bank statements) za miezi mitatu inayoishia Juni 2019.
8. Kivuli cha Taarifa za Kampuni (Company Profile) kwa makampuni tu.
9. Wadhamini wawili wenye barua za utambulisho kutoka kwa mtendaji wa mtaa anapoishi.

**MASHARTI KWA MWOMBAJI:**

1. Mwombaji awe mmiliki wa Kampuni ya usafirishaji wa mabasi au wakala wa usafirishaji wa mabasi anayetambuliwa na mmiliki wa Kampuni anayofanyia Kazi (Kampuni zitapewa vipaumbele)
2. Ifahamike wazi kuwa mwombaji atalazimika kutumia kibanda atakachopangishwa na Halmashauri kwa matumizi ya kutoa huduma ya kukata tiketi kwa abiria tu na si vinginevyo
3. Fomu ya maombi iambatane na nakala ya vielelezo vinavyohitajika
4. Kupangisha chumba kwa mtu wa tatu haitaruhusiwa katika kipindi chote cha mkataba
5. Mwombaji atakayeshinda zabuni atapeleka kodi ya kila mwanzo wa mwezi katika Benki ya **NMB** (**Own Source Collection Account no: 51610000197**) Mpangaji atatakiwa kupeleka kodi yote kwa kila mwezi. (kama huna uhakika wa kulipa kodi iliyotajwa usiombe chanzo husika).
6. Kampuni ya usafirishaji / wakala wa usafirishaji ambaye alishawahi kupanga jengo la Manispaa ya Kigoma/Ujiji na **KUSHINDWA** kulipa kodi kwa mujibu wa Mkataba au kuvunja masharti yoyote ya mkataba kama vile kufanya udanganyifu **HARUHUSIWI** kuomba kuwa Mpangaji.
7. Mshindi wa Zabuni ya husika atawajibika kufanya usafi wa eneo la kazi na kupeleka takataka eneo la kukusanyia taka.
8. Mwombaji ataje kodi/ gharama atakayolipia kwa mwezi
9. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka dhamana (bond) kiasi sawa na bajeti ya miezi mitatu (3) kabla ya kuanza kupanga ambayo mpangaji atarudishiwa baada ya ukomo wa mkataba endapo atakuwa hana deni lolote au kuwasilisha hati original ya nyumba, udhamini benki (bank guarantee).Hutakabidhiwa chumba bila ya kuweka dhamana (bond).
10. Viwango vilivyopangwa vya fedha vinaweza kubadilika muda wowote kulingana na mabadiliko ya sheria mpya au kutokana na maelekezo ya serikali.
11. Mpangaji atakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za changamoto anazokutana nazo kwa meneja wa stendi na kwa Mkurugenzi wa Manispaa.
12. Mpangaji atakuwa na wajibu wa kuwasilisha kwa Meneja wa mapato, kopi ya stakabadhi ya malipo (ya mfumo wa mapato) aliyofanya benki.
13. Kila mwombaji atalipa ada ya maombi ya zabuni ambayo haitarudishwa na kila ombi ni zabuni inayojitegemea na italipiwa kiasi cha ada kilichoainishwa katika

13. Kila mwombaji atalipa ada ya maombi ya zabuni ambayo haitarudishwa na kila ombi ni zabuni inayojitegemea na italipiwa kiasi cha ada kilichoainishwa katika **akaunti na. 51610000197 NMB kwa jina la Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.**
14. Watakaopata zabuni watatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
15. Bodi ya zabuni haitalazimika kukubali zabuni ambayo gharama zake ziko juu au chini sana. (Atakayekidhi vigezo vya sheria ya manunuzi ndiye atakaepewa kazi na Bodi ya zabuni).
16. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha zikiwa ni **"ORIGINAL MOJA NA COPY MBILI"** (kwa Lakiri). Juu ya bahasha ioneshe aina ya zabuni, namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

    **Katibu wa Bodi ya Zabuni,**

    **Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji,**

    **S.L.P. 44, KIGOMA**

17. Kwa maelezo zaidi kuhusiana na zabuni hizi, fika katika Ofisi za Halmashauri ya Manispaa zilizopo eneo la Mnarani muone Katibu wa Bodi ya Zabuni.
18. Fomu za maombi ya zabuni zinapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU) ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.
19. Vigezo vya tathmini ya zabuni zote ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya zabuni hizo ni **Alhamis ya tarehe 4 September 2019** ambayo ndiyo itakuwa siku ya ufunguzi wa zabuni hizo saa **5.00 asubuh**i, katika ukumbi wa **Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji.** Mwombaji au mwakilishi wake wanakaribishwa katika ufunguzi wa zabuni hizo.

Mwailwa S. Pangani
**Mkurugenzi wa Manispaa**
**KIGOMA UJIJI**

MKURUGENZI WA MANISPAA
KIGOMA/UJIJI